



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MANISPAA YA
MOSHI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.MMC/A.40/29/VOL.II/84

Tarehe: 30/05/2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kuomba nafasi ya kazi iliyotajwa hapo chini, baada ya kupokea kibali chenye Kumb. Na. FA .228/613/01/B/073 cha tarehe 02.04.2024 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1 DEREVA II- (NAFASI 1)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe na cheti cha kidato cha nne (form iv) na Leseni ya Daraja C au E ya uendeshaji magari.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (log book).
- vi. Kufanya usafi wa gari.
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

2.2 MSHAHARA

Ngazi ya mshahara ni TGS B1

3.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
- iii. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishwe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili ambavyo ni vyeti vya **Kidato cha Nne, Kitado cha Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Cheti cha Kompyuta, Vyeti vya kitaaluma (Professional Certificates from respective boards) "Testimonials", Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- vii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na **CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010**.
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe, **12/06/2024**.
- x. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisa barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

Mkurugenzi Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa
S.L.P 318,
MOSHI-KILIMANJARO

- Xi Maombi yote yatumwe kwenye Mfumo wa kieletroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia Anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal")
- xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tângazo hili HAYATAFIKIRIWA.
- Xiii. Limetolewa na:


MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
S.L.P 318
MOSHI.